

Mreno awanyweshwa mtindi wananchi waumbue Frelimo

MRENO katika Msumbiji akiwa katika juhudi yake ya kuwatesa wananchi, sasa anawakamata na kuwanyweshwa mtindi wa kizungu uitwao 'Kunyake' na walewapo huwauliza maswali juu ya siasa ya Frelimo. Jamaa hao huanza kubwata ovyo na hatimaye wanapewa mateso makali sana kama wanyama.

Taarifa motomoto kutoka Msumbiji inasema kwamba wananchi wapatao mia na themanini na sita wametiwa nguvuni na Serkali ya Mreno. Sababu ya kukamatwa kwao ni kwamba iamaa hao walijitolea kabisa katika mambo ya siasa ili kumwondoa mkoloni wao Mreno,

Kwa vile Mreno hataki kabisa kusikia neno la siasa anawatesa sana wanauchi hao kwa njia mbalimbali mbali na hasa kwa mapigo na wengine wao wameumizwa vibaya na wengine wakawahi kuzimia na kupelekwa hospitalini. Taarifa hiyo inaendelea kusema kwamba hakuna tumaini lo lote juu ya maisha ya wananchi hao kwani

Nguzungu 8/8/63

wengi wao wanaonekana na hali mbaya sana ndani ya hospitali ya Wilaya ya Mueda katika Jimbo la Cabo-Delgado.

Majeshi yavinjari

Jamaa hawa wanaokamatwa wanapelekwa kwenye Jela kuu ya mateso huko Lourenco Marques, mji mkuu wa Msumbiji.

Majeshi ya Kireno kutoka Libson ambayo yanaletwa na Salazaar yameyazunguka majimbo yote ya Msumbiji wakiwa na zana za vita, na ndege za kivita zina-
vinjari angani kando-
kando ya bahari na mto wa Ruvuma ili kuzuia watu wasiweze kutoroka kwenda nchi zingine kwa kuokoa maisha yao.

Kunyake